


(II) Ngazi ya Wilaya

MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA WILAYA YA MAGU
Umetolewa: 24/08/2023

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Magu.

 <p>Kielelezo ■ Juu ya wastani hadi wastani</p>	<p>Dondoo muhimu</p> <ol style="list-style-type: none"> Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Magu. Mvua zitaanza wiki ya pili ya Oktoba, 2023. Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2024. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.
<p>Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 kwa wilaya ya Magu, Mwanza.</p>	

<p>Mvua za msimu wa Vuli, 2023 kwa wilaya ya Magu</p> <p>Zitaanza: Wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.</p> <p>Zitaisha: Mwezi Januari, 2024.</p> <p>Kiasi cha mvua zinazotarajiwa: Mvua zinatarajiwa kuwa juu ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Magu ni kati ya milimita 320 hadi 410.</p> <p>Kiwango cha juu cha mvua: Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2023.</p> <p>Vipindi vya ukavu: Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2023.</p> <p>Ulinganifu: Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.</p> <p>Angalizo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. 	<p>Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi</p> <p>Matokeo</p> <ol style="list-style-type: none"> Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza. Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo. Upatikanaji wa chakula cha Samaki na malisho ya mifugo unatarajiwa kuongezeka. <p>Ushauri</p> <ol style="list-style-type: none"> Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi. Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa. Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.
--	--

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz